



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA



Kumb. Na.LD/MK/10151/10


11/02/2025

Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA)

S.L.P 6775,

Dar Es Salaam.



**YAH: KIWANJA NA. 10 KITALU 'W' MWANAMBAYA, WILAYA YA MKURANGA**  
Rejea mada tajwa hapo juu,

2. Ninachukua fursa hii kuijulisha Ofisi yako kwamba, Kampuni ya **Mwangamkali Company Limited** imenunua kiwanja tajwa na sasa wanatakiwa kusajiliwa na kupewa cheti cha usajili wa mradi na Ofisi yako.

3. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999, fungu la 19-20, Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, Kanuni za Ardhi za 2001, kanuni ya 9C (v), kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA).

4. Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi kwako ili iweze kupatiwa Certificate of Incentives kwa kuwa kiwanja hiki ni halali na hakina mgogoro wowote.

5. Naomba kuwasilisha kwa hatua zako muhimu.

Godson W. Mushi

K.n.y: Mkurugenzi Mtendaji (W),

Mkuranga.



**Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Mkuranga-----Kwa taarifa**

Mwangamkali Company Limited

Dar es salaam--- kwa ufuatiliaji